

١٦ ربيع أول ١٤٤٣ هـ
٢٢ أكتوبر ٢٠٢١ م

جمهورية مصر العربية
وزارة الأوقاف

(١)

النبي (ص) معلما ومرييا

Mtume S.A.W, Mwalimu na Mlezi.

Imefasiriwa na

Profesa.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa Viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitukufu:

{فِيمَا رَحْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ}

{Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao}.

Na ninashuhudia ya kwamba hakuna Mungu mwingine yoyote isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ninashuhudia ya kwamba Mtume Muhammad S.A.W ni Mja na Mtume wake. Ewe Mola wetu Mlezi mpe rehema na amani na umbariki yeye na Jamaa zake wote na Maswahaba wake wote, na kila mwenye kuwafuata kwa wema mpaka Siku ya Malipo.

Na baada ya Utangulizi huu,

Ndugu zangu waislamu kwa hakika Mtume S.A.W alikuwa Ruwaza ya Juu ya kuigwa na Binadamu wote katika malezi ya hali ya juu na ufundishaji mzuri kuliko wowote, Mtume S.A.W alikuwa Mwalimu Mwenye huruma, Mlezi mwenye hekima anafundisha hatua kwa hatua na anaelimisha kwa Wema, na hasa kwa kuwa yeye S.A.W, ndiye anayesema (إِنَّ اللَّهَ لَمْ يَبْعِنِي مُعْتَنًا، وَلَا مُتَعَتَّنَا، وَلَكِنْ بَعَّنِي مُعَلِّمًا، وَمَيْسِرًا) :

(Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hakunituma mimi nifundishe ukaidi au niwe mkaidi, bali amenituma mimi niwe mwalimu mwepesishaji). Na Mtume S.A.W, anasema:

(٢)

(إِنَّ الرُّفْقَ لَا يَكُونُ فِي شَيْءٍ إِلَّا زَانَهُ، وَلَا يُزْعُ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا شَانَهُ)

(Hakika upole hauwi katika kitu isipokuwa hukipendezesha kitu hicho na hauondoshwi katika kitu isipokuwa hukifanya kitu hicho kiwe kibaya)

Na mzingativu wa Sira ya Mtume S.A.W, atakuta kuwa Mtume ni mwalimu bora wa Maswahaba wake R.A, na kwa watu wote, na kwamba Mtume S.A.W, ni Mpole mno katika Viumbe kwa Viumbe, na ni mwenye kiwango cha huruma cha juu mno kwa wale anaowafundisha, anaewaadabisha na kuwaelekeza. Tunamwona Muawiya bin Hakam R.A, anasema: Nilipokuwa ninasali na Mtume S.A.W, Mtu mmoja alipiga chafya nikasema: Yarhamuka Allaahu (Mwenyezi Mungu akurehemu), watu wote wakanikodolea macho, nikasema: mna nini nyinyi? Mbona mnaniangalia hivyo? Wakawa wanajipiga mapajani kwa mikono yao, nilipoona kuwa wananinyamazisha nilinyamaza. Na Mtume alipomaliza kusali sala yake, Hakika yeye ni kama baba na mama yangu, sijawahi kumwona mwalimu kama yeye, kabla yake na baada yake anaejua kufundisha vizuri kama yeye. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, Mtume hakunitenza nguvu, wala hakunipiga, wala hajanitukana, akasema: (إِنَّ هَذِهِ الصَّلَاةَ لَا

يَصْلُحُ فِيهَا شَيْءٌ مِنْ كَلَامِ النَّاسِ، إِنَّمَا هِيَ التَّسْبِيحُ، وَالتَّكْبِيرُ، وَالتَّهْلِيلُ، وَقِرَاءَةُ الْقُرْآنِ).

(Hakika hii sala haifai ndani yake maneno ya watu, Hakika hii sala ni kumsabihi Mwenyezi Mungu (kusema subhaanallah), na kutoa takbira (kusema Allaahu Akbar), na kutoa Tahlili (ni kusema laa ilaaha illa Allaahu) na kusoma Qurani Tukufu.

Ndugu zangu waislamu huyu ni mtume wa rehema

Na kutoka kwa Abu Amamah R.A, amesema: Kijana mmoja alikuja kwa Mtume S.A.W, kwaoja mdogo akasema: Ewe Mtume wa

(٧)

Mwenyezi Mungu nipe idhini ya Uzinzi. Watu wakamgeukia yule Kijana, na wakamkemea, wakasema: nyamaza, nyamaza. Akasema: msogezeni karibu. Wakamsogeza karibu kisha akamwambia: kaa na akakaa, akasema: Je unakipenda kitendo hicho afanyiwe mama yako? Akasema: hapana kwa kweli. Mwenyezi Mungu anijaalie nijitolee kwa ajili yako. Akasema Mtume S.A.W, Na Watu wote hawapendi kitendo hicho wafanyiwe mama . Kisha akamuuliza: Je, unapenda kitendo hicho afanyiwe binti yako? Akasema hapana kwa kweli Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anijaalie niwe fidia kwako. Na Watu wengine pia hawapendi Kitendo hicho wafanyiwe mabinti zao. Akamuuliza: Je, unapenda kitendo hicho afanyiwe Dada yako? Hapana kwa kweli. Mwenyezi Mungu anijaalie niwe fidia kwako. Na Watu wengine pia hawapendi kabisa kitendo hicho kwa dada zao. Akamuuliza: Je, unapenda afanyiwe hivyo Shangazi yako? Akasema Hapana kwa kweli. Mwenyezi Mungu anijaalie niwe fidia kwako. Na Watu wote pia hawapendi kabisa kwa Shangazi zao. Akamuuliza: Je, unapenda kitendo hicho kwa Mama yako mdogo? Akasema: Hapana kwa kweli. Mwenyezi Mungu anijaalie niwe fidia kwako. Akasema: Watu wote hawapendi Kitendo hicho kwa Shangazi zao. Akasema: Mtume akaweka mkono wake juu yake kisha akasema: Ewe Mola wetu Mlezi msamehe dhambi zake, na uisafishe moyo wake na uulinde utupu wake.

Yule kijana baada ya hapo hakuwa ni mwenye kuangalia chochote cha kumtanisha.

Na mwisho wa hutoba hii namwomba Mwenyezi Mungu Aniongoze mimi na nyinyi na Anighufiri mimi na nyinyi mtupeni yarhamukum

Allah

(٤)

Na katika hotuba hii ya pili tunazungumza juu ya mtindo wa Mtume wetu katika mafundisho yake ya kidaawah na kielimu.

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa Viumbe vyote, na Sala na Salamu zimwendee Mtume wa Mwisho, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Ndugu zangu waislamu

Hakika mzingativu wa Maisha ya Mtume wetu S.A.W, ataona kuwa Mtume mara nyingi alikuwa na shime ya kuwa na njia nyingi za Kulingania na Kufundishia, na anatumia stadi zake zote za Mawasiliano ya Kiulinganiaji; ili aweze kuingia katika akili ya mwenye kujifunza pamoja na kuingia moyoni mwake. Baadhi ya nyakati Mtume S.A.W alikuwa anatumia lugha ya namba kwa ajili ya kuzijongolesha akili kwa

mujibu wa Kauli yake S.A.W: **ثَلَاثٌ مَنْ كُنَّ فِيهِ وَجَدَ حَلَاوَةَ الْإِيمَانِ: أَنْ يَكُونَ اللَّهُ وَرَسُولَهُ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِمَّا سِوَاهُمَا، وَأَنْ يُحِبَّ الْمَرْءَ لَا يُحِبُّهُ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنْ يَكْرَهُ أَنْ يَعُودَ فِي الْكُفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْقَذَهُ اللَّهُ مِنْهُ؛ كَمَا يَكْرَهُ أَنْ يُلْقَى فِي النَّارِ**

(Mambo matatu akiwa nayo Mtu basi atakuwa ameupata utamu wa Imani: Mwenyezi Mungu na Mtume wake wawe vipenzi zaidi kuliko wengine wowote wasio kuwa hao wawili, na ampende Mtu, na hampendi isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na achukie kurejea ukafirini baada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kumwokoa na ukafiri huo, kama achukiavyo kutoswa Motoni).

Na wakati mwingine Mtume anafundisha kwa kutoa mifano fafanuzi:

kama vile kauli yake Mtume S.A.W: **إِنَّمَا مَثَلُ الْجَلِيسِ الصَّالِحِ، وَجَلِيسِ السُّوءِ، كَحَامِلِ الْمِسْكِ، وَنَافِخِ الْكَبِيرِ، فَحَامِلُ الْمِسْكِ إِذَا أُنْزِلَ يَحْدِيكَ، وَإِنَّمَا أُنْزِلَ مِنْهُ، وَإِنَّمَا أُنْزِلَ مِنْهُ رِيحًا طَيِّبَةً، وَنَافِخُ الْكَبِيرِ إِذَا أُنْزِلَ يَحْرِقُ ثِيَابَكَ، وَإِنَّمَا أُنْزِلَ مِنْهُ رِيحًا خَبِيثَةً.**

(Hakika mfano wa Mtu mzuri wa kuketi naye na Mtu mbaya wa kuketi naye ni kama mbeba Miski na Muhunzi, kwani mbeba Miski ima akakupa harufu nzuri au ukanunua miski kutoka kwake au ukapata harufu nzuri kutoka kwake, na Muhunzi huwenda akakuunguzia nguo zako au huwenda ukapata harufu mbaya kutoka kwake).

Na katika baadhi ya nyakati Mtume S.A.W alikuwa anatomia njia ya kuuliza maswali, ili kumtia shauku msomaji na kumzindua, na katika hilo, kauli yake Mtume S.A.W:

أَتَدْرُونَ مَنْ الْمُفْلِسُ؟ قَالُوا: الْمُفْلِسُ مَنْ لَا دِرْهَمَ لَهُ وَلَا مَتَاعَ، فَقَالَ (صلى الله عليه وسلم): إِنَّ الْمُفْلِسَ مِنْ أُمَّتِي يَأْتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِصَلَاةٍ وَصِيَامٍ وَزَكَاةٍ، وَيَأْتِي قَدْ شَتَمَ هَذَا وَقَذَفَ هَذَا، وَأَكَلَ مَالَ هَذَا، وَسَفَكَ دَمَ هَذَا، وَضَرَبَ هَذَا فَيُعْطَى هَذَا مِنْ حَسَنَاتِهِ، وَهَذَا مِنْ حَسَنَاتِهِ، فَإِنْ فَنِيَتْ حَسَنَاتُهُ قَبْلَ أَنْ يُقْضَى مَا عَلَيْهِ أَخَذَ مِنْ خَطَايَاهُمْ فَطُرِحَتْ عَلَيْهِ، ثُمَّ طُرِحَ فِي النَّارِ.

(Je, mnamjua mtu aliyefilisika? Wakasema: Mtu aliyefilisika ni yule asiye na mali au hamiliki chochote, akasema Mtume S.A.W: Hakika Mtu aliyefilisika katika Umma wangu atakuja siku ya Kiama akiwa na Swala, na Swaumu na Zaka, na anakuja hali ya kuwa alimtukana huyu, alimsingizia uzinzi yule, na alikula mali ya huyu na akamuua huyu na akampiga huyu. Basi mtu huyu anapewa katika mema yake, na huyu

(٦)

anapewa katika mema yake, na ikiwa mema yake yataisha kabla ya kuwalipa wale wanaomdai basi maovu yao yatachukuliwa kisha atstupiwa yeye, na kisha akatupwa Motoni).

Vilevile Mtume S.A.W alikuwa akizichagua siku na nyakati zinazofaa kwa ajili ya kuelimisha na kuelekeza, kwa kuchangamsha akili za anaowafundisha, na kwa lengo la kuwaondoshe mchoko , ambapo anasema Bwana Wetu Abdallah bin Masoud R.A: Mtume S.A.W alikuwa akituahidi sisi kwa ajili ya mawaidha katika siku maalumu kwa kuchelea tusichokeshwe.

Haja iliyoje kwetu sisi tuyafuate maadili ya Mtume wetu S.A.W, tukiyafunza na kujifunza, kwa ajili ya kueneza Ujumbe wake na kuweka wazi Mwongozo wake na Sunna zake.

Ewe Mola wetu Mlezi tunakuomba uturuzuku Elimu na Adabu, na utuongoze katika kujipamba na Maadili ya Mtume wetu S.A.W.

Na mwisho wa daawa yetu ni Alhamdulillah.